

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



Ofisi ya Uthibiti Ubora wa Shule,
Wilaya ya Iringa,
S.L.P 984,
IRINGA.
31/05/2019.

TANGAZO LA KUTAFUTA MAFUNDI UFYATUAJI TOFALI ZA SARUJI (BLOCKS) KWA AJILI YA KAZI YA UJENZI WA OFISI YA MTHIBITI MKUU UBORA WA SHULE WA WILAYA YA IRINGA.

Kazi Na. UKW/IRV/V.2002/UJ/OUT/03

Mthibiti Mkuu Ubora wa Shule (W) Iringa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa imepokea fedha kutoka Serikali kuu kwa ajili ya Ujenzi wa ofisi ya Mthibiti Ubora wa Shule wa Wilaya ya Iringa. Ujenzi utatekelezwa kwa utaratibu wa "Force account". Hivyo, Mthibiti Mkuu Ubora wa Shule (W) Iringa anawatangazia Mafundi na vikundi vyenye uwezo wa kufyatua matofali ya saruji (Blocks) kwa kutumia mashine ya Mkono na umeme kuleta maombi yao.

Maombi yanakaribishwa kwa kikundi au Fundi mwenye sifa zifuatazo:-

1. Fundi awe na mashine yenye uwezo wa kufyatua tofali yenye vipimo nchi sita (6) (Urefu x Upana x Unene) = (450mm x230mm x150mm)
2. Fundi awe na uzoefu wa kufyatua tofali za saruji (blocks) ishirini na tano (25) kwa mfuko mmoja wa saruji kwa ubora unaotakiwa.
3. Fundi ataje idadi/ uwezo wa tofali anazoweza kufyatua kwa siku.
4. Fundi ataje gharama za kufyatua tofali 1 la saruji (blocks) ikijumuisha gharama zake zote. (N.B: Vifaa, mchanga, saruji, maji, vibarua na mwajiri)

5. Endapo fundi atafyatua tofali za saruji (blocks) zilizo chini ya kiwango kwa uzembe atalazimika kulipa gharama za vifaa vilivyotumika.
6. Fundi aoneshe idadi anzia ya tofali atakazohitaji kulipwa baada ya kuzifyatua.
7. Matafali yatalipwa baada ya kukaguliwa na Mhandisi na Kamati ya Ukaguzi na Mapokezi.
8. Fundi atalazimika kumwagilia maji (Curing) tofali alizofyatua kwamuda usiopungua siku saba (7) mfululizo.
9. Fundi awe tayari kufanya kazi katika eneo la ujenzi wa Ofisi ya Mthibiti Mkuu Ubora wa Shule -Mawelewele karibu na Mskiti wa ASAS, Manispaa ya Iringa.
10. Mafundi watakao omba kazi hii wakiwa kwenye vikundi watapewa kipaumbele Zaidi.
11. Fundi awasilishe uthibitisho wa kutokuwa ametenda kosa la kijinai, kuwa na mgogoro na serikali
12. Fundi atatakiwa kuonesha uthibitisho wa kuwa na vitendea kazi muhimu vitakavyo mwezesha kukamilisha kazi husika. Angalau mashine mbili (2) na vibao vyenye vipimo sawa.
13. Fomu ya ufyatuaji tofali inapatikana katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi (PMU), MAKAO MAKUU YA WILAYA YA IRINGA, S.L.P 108, IRINGA) iliyopo katika Jengo la SIASA NI KILIMO, MTAA WA GANGILONGA, kuanzia tarehe 31/05/2019 hadi tarehe 06/06/2019. Katika muda wa kazi kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri, Jumatatu hadi Ijumaa.
14. Maombi ya kazi ya ufyatuaji wa tofali za saruji (blocks) yatawasilishwa kwa kujaza fomu ya ufyatuaji tofali na kuambatishwa pamoja na barua ya maombi.
15. Maombi ya kazi ya ufyatuaji wa tofali za saruji (blocks) ya andikwe kwa herufi kubwa yakionesha aina ya kazi uliyoomba, Jina la fundi au

Kikundi na yawekwe kwenye bahasha isiyo na mchoro wala alama yoyote na yafungwe kwa lakili. Aidha bahasha ifungwe vizuri. Pia juu ya bahasha iandikwe jina la kazi uliyoomba. Namba ya kazi husika na anuani ya (KATIBU WA KAMATI YA MANUNUZI, UJENZI WA OFISI YA MTHIBITI MKUU UBORA WA SHULE WA WILAYA YA IRINGA, S.L.P 984, IRINGA)

16. Maombi yote katika nakala halisi moja (1) na nakala kivuli moja(1) yaletwe kwenye Ofisi ya Manunuzi na Ugavi (PMU), MAKAO MAKUU YA WILAYA YA IRINGA, S.L.P 108, IRINGA) iliyopo katika Jengo la SIASA NI KILIMO, MTAA WA GANGILONGA. Muda wa kazi kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri.
17. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi hayo ni tarehe 06/06/2019, saa 4.00 asubuhi na maombi hayo yatafunguliwa hadharani mara tu, baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha.
18. Maombi yote ya kazi za ufyatuuji tofali za saruji (blocks) yatakayowasilishwa baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha hayatapokelewa.
19. Siku ya kutembelea eneo la mradi ili kuwezesha kujaza makabrasha itakuwa tarehe 01/06/2019 (Jumamosi). Waombaji wote wafike saa 3.00 kamili asubuhi katika jengo la SIASA NI KILIMO – Gangilonga ili kwenda kuona eneo ulipo mradi Mawelewele karibu na msikiti wa ASAS, kuanzia saa 3.00 kamili asubuhi. Gharama za kutembelea eneo la mradi kila mwombaji atajitegemea.
20. Waombaji wote wanaombwa kuhudhuria katika ufunguzi wa kazi hii katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

.....
**MWENYEKITI WA KAMATI YA UJENZI
OFISI YA MTHIBITI MKUU UBORA WA SHULE
WILAYA YA IRINGA**